Hati hii inaeleza kwa muhtasari msimamo, maongozi na maku-sudio ya Chama cha KANU kuhusu maendeleo ya wananchi wa Kenya. Maongozi ya Chama na Serikali yameleta mafanikio makubwa tangu tulipojinyakulia uhuru.

Hata hivyo, tuna wajibu muhimu wa kutimiza. Matatizo yana-yotukabili katika kutimiza wajibu huo ni makubwa. Tuna nafasi nzuri za kuleta maendeleo. Wajibu wetu muhimu ni kutambua nafasi hizo na kuhakikisha kwamba tunazitumia vyema kuimarisha umoja na maendeleo ya Taifa letu.


Tangu tulipojinyakulia uhuru Chama cha KANU kimethibitisha uaminifu wake wa kuwatimizia wananchi ahadi zake. Serikali ya KANU ni Serikali ya vitendo na haifuati uvumi usio na maana. Jambo lililo muhimu sasa ni kutekeleza mpango wetu wa kuzifanya wilaya kuwa msingi wa maendeleo. Mpango huo utahakikisha kwamba wananchi watashirikiana na kuungana na Serikali pamoja na Chama kuendesha mipango ya maendeleo. Kila juhudi itafanywa kuharakisha maendeleo ya wilaya zote. Tutahakikisha kwamba akiba ya pesa zetu, mali yetu ya asili na ujuzi wa wananchi vita-tumiwa kwa maendeleo na kwa manufaa ya Taifa letu kwa jumla.

Chama cha KANU ndicho chombo muhimu cha siasa na nguzo ya maendeleo ya Taifa letu. Chama cha KANU kitachukua hatua bila kusita ama kukawia mara tu dalili za matatizo zinapoonekana. Kwa hivyo tutazingatia imani ya kuwa Chama cha wananchi, chenye vitendo katika kila tawi. Katika jitihada za kukiongezea nguvu Chama chetu, mipango ya kushirikisha sehemu mbalimbali za wananchi iko tayari. Tutahakikisha kwamba wazee, vijana, watu wenye ujuzi na wananchi wengineo watashiriki katika mashauri na kazi za Chama.

Jambo muhimu ninalotaka wananchi wote wa Kenya walifahamu katika muda huu tunaotarajia uchaguzi wa wabunge na madiwani, ni kwamba maongozi ya nchi yetu yamo mikononi mwa wananchi. Ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kwamba tuna umoja, tunapendana, na kwamba tunaishi kwa amani.

Yaani, tufuate maongozi ya Nyayo ya Amani, Upendo na Umoja.

HARAMBEE!!! NYAYO!!!

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Jaramba Rais'. The signature is fluid and cursive, with a long horizontal stroke at the beginning and a smaller, more compact signature to the right.

Rais.

KANU

Tumeahidi katika Chama cha KANU kuhifadhi, kuimarisha na kulinda Katiba ya Kenya. Katiba hiyo ndiyo inayoeleza na kuhifadhi sheria, haki na masharti ya kila mwananchi.

Katika Chama cha KANU tunaamini maongozi ya kidemokrasia yanayohakikisha haki ya wananchi ya kujichagulia Rais na viongozi wote wanaowawakilisha katika Bunge na mabaraza mengineyo.

Tangu tulipojinyakulia uhuru tumethibitisha kwamba demokrasia ya Chama kimoja inawezekana na ni msingi muhimu wa amani na maendeleo yanayofaa. Kwa hivyo Chama cha KANU kimefanywa kuwa Chama cha pekee katika Katiba yetu.

Serikali ya KANU itaendelea kuhifadhi na kulinda haki na sheria zetu na kuhakikisha uhuru wa mahakama.

MSIMAMO

Katika juhudi za kupanga, kutayarisha na kutekeleza mipango ya maendeleo ya nchi yetu, Serikali ya KANU inaamini kwa dhati kwamba maendeleo yoyote yanayoleta manufaa kwa wananchi ikiwa yamebuniwa na watu binafsi, vyama vya ushirika ama Serikali ni lazima yatiliwe mkazo.

Katika kutimiza wajibu huo :

- (i) Serikali itashirikiana na wananchi kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo wilayani.
- (ii) Serikali itaendelea kujishughulisha zaidi na mambo inayoweza kukamilisha kwa njia bora na kuwachia watu wengine yale wanayoweza kuyafanya kwa njia bora.
- (iii) Wananchi wanaonufaika na huduma za Serikali watahitajiwa kulipia sehemu ya gharama za huduma hizo.
- (iv) Serikali inafaa isaidie wananchi ili waweze kujisaidia wenyewe.
- (v) Serikali na wananchi kwa jumla lazima wahakikishe kwamba vifaa tulivyo navyo sasa vinatumiwa kwa njia bora na kwa ukamilifu na kuhifadhiwa kwa njia inayofaa.
- (vi) Serikali itaanzisha taratibu ya mwenendo kwa watu wote.
- (vii) Serikali itahakikisha kwamba kila mwananchi ananufaika kutokana na matunda ya maendeleo.

UTUMISHI WA SERIKALI

Kifaa chenye maana kuliko vifaa vingine vyote vya Serikali ni watumishi wake.

Kwa hivyo, Serikali itajitahidi kuimarisha ustadi na uaminifu wa watumishi wake.

Idadi ya wafanyikazi wa Serikali pamoja na walimu imeongezeka kuanzia 183,500 mwaka wa 1971 hadi 337,000 mwaka huu. Jambo la kwanza lililo muhimu ni kuchunguza idadi na aina ya wafanyikazi hao.

Wafanyikazi watakaoajiriwa kusimamia mipango ya maendeleo, wataajiriwa kufuatia sheria za idara inayosimamia wafanyikazi wa Serikali.

Idara inayosimamia wafanyikazi wa Serikali itaimarishwa ili iweze kupanga wafanyikazi kulingana na ujuzi walio nao na mahitaji ya uchumi wetu.

Katika kuongeza ujuzi wa watumishi wake, Serikali itafikiria kwanza wafanyikazi wanaosimamia maendeleo ya nchi hii.

Imedhihirika wazi kwamba kanuni zinazofuatwa kuwapandisha vyeo wafanyikazi wa Serikali zinahitaji kurekebisha ili wafanyikazi wanaostahili kupewa madaraka wapate vyeo hivyo inavyopasa.

Kamati maalum itaundwa kuchunguza sheria zinazotumika kuwadhibu wafanyikazi wanaokosea sheria za watumishi wa Serikali, hasa udanganyifu unaohusu pesa, ili wadhibiwe mara tu wakipatikana.

IDADI YA WATU

Idadi ya watu na shughuli za kupanga uzazi ni sehemu mojawapo iliyo muhimu katika mila za Kiafrika.

Serikali ya KANU itaendelea na jitihada za kuimarisha shughuli za kupanga uzazi kwa kutumia njia za kisasa na pia za kienyeji. Serikali itahakikisha kwamba idadi ya watu inaongezeka kufuatana na uwezo wa uchumi wetu wa kuwatimizia wananchi mahitaji yao.

Idadi ya watu inaongezeka kwa asilimia tatu na nukta nane kwa mwaka. Maongezeko hayo hayalingani na uwezo wa uchumi wetu. Ni wazi kwamba tukipanga maendeleo yetu ya kuongeza chakula, huduma ya afya, elimu na viwanda itatubidi pia tupange uzazi na maongezeko ya watu.

ARDHI

Serikali ya KANU itaendelea kuzingatia mpango wake wa ugawanyaji wa ardhi na kuandikisha hati za kumiliki ardhi.

Serikali itaendelea kuwa na mashamba yake maalum ya utafiti, kulea mifugo bora, kutoa mbegu bora, kuonyesha aina mpya za maarifa, na kwa vituo vya mafunzo ya wakulima.

Shughuli za kuwapatia wananchi makao katika sehemu zilizo-kuwa zimetengwa kutumiwa na wakoloni ziko karibu kukamilika.

Serikali ya KANU sasa itashughulika na mambo matatu muhimu:

- (i) Ukulima bora katika sehemu zilizo na rutuba ya kutosha.
- (ii) Kustawisha sehemu zilizo kavu ambazo zinaweza kufaa kwa ufugaji na ukulima.
- (iii) Kueneza mpango wa kunyunyizia maji mashambani katika sehemu zilizo karibu na Ziwa Victoria, mito ya Athi na Tana, bonde la Kerio, na sehemu nyinginezo zilizo na maji ya kutosha.

Mipango ya kuhifadhi udongo itakaririwa na kufanywa kuwa shughuli muhimu katika sehemu za mashambani.

MALI YA ASILI

Sehemu ya eneo la Kenya iliyo na misitu ni hekta 1,365,360, ambayo ni asilimia tatu tu ya eneo lote la Kenya.

Ni wazi kwamba nia yetu ni lazima iwe ya kuongeza eneo la misitu humu nchini. Jumla ya miche ya miti milioni 85 ilipandwa mwaka wa 1982. Inatulazimu tujipangie kiwango cha kupanda miti milioni 200 kila mwaka.

Inatulazimu tupande aina ya miti inayokuwa haraka.

Serikali itasimamia kiasi cha miti inayokatwa kwa sababu kiasi cha miti inayotumia kupikia ni kikubwa kupita kiasi cha miti inayoweza kukatwa bila kuangamiza misitu yetu.

Inatubidi tuendelee na jitihada zetu za kuchunguza aina ya miti inayofaa kupandwa sehemu mbalimbali humu nchini.

Tutaendelea na jitihada zetu za kutafuta mafuta na aina nyingine za mali ya asili katika sehemu zote za Kenya.

NGUVU ZA UTENDAJI

Katika nguvu za utendaji tunazotumia humu nchini ni asilimia kumi na saba tu itokayo humu nchini. Sehemu kubwa ya asilimia themanini na tatu ni mafuta kutoka nchi za nje. Asilimia hamsini na tano ya pesa zetu za kigeni zinatumiwa kununua mafuta hayo.

Ni wazi kwamba inatubidi:

- (i) Kujitahidi kuhifadhi nguvu za utendaji.
- (ii) Tutafute aina nyingine za nguvu za utendaji zinazoweza kutumika zaidi ya mara moja.
- (iii) Kustawisha kwa ukamilifu nguvu za umeme, zitokanazo na kinyesi, na pia kuhifadhi na kuongeza misitu yetu. Misitu hutupatia kuni zinazotumiwa na asilimia themanini ya wananchi wote wa Kenya wanaoishi sehemu za mashambani.

HAZINA

Kwa miaka iliyopita wananchi wa Kenya wamekuwa wakitenga sehemu ya asilimia ishirini ya mapato yao kwa mipango ya uchumi.

Lengo letu hasa ni kuhakikisha kwamba Serikali, ushirika na watu binafsi wananufaika sawa kutokana na mikopo.

Mipango ya kuwajiri kazi wananchi kuchukua nafasi za kazi zinazohusu uchumi zinazoshikiliwa na wageni itaharakishwa.

Sheria mpya itafikishwa Bungeni hivi karibuni kuhakikisha kwamba akiba zinazotolewa na wananchi kwa kampuni za bima zinatumiwa kuimarisha maendeleo ya nchi yetu.

Kamati maalum itaundwa kuhakikisha kwamba wakulima na wafanyi biashara wanaokopa kutoka kwa mashirika ya Serikali wanalipa mikopo yao bila kuchelewa.

Mashirika yanayohusika na pesa yatahimizwa kukopesha sehemu kubwa ya akiba yao kwa shughuli za kilimo na maendeleo ya sehemu za mashambani.

Serikali ya KANU itaendelea kuchunguza faida ya kuweka akiba na kuwahimiza wananchi waongeze sehemu ya mapato yao wanayoweka akiba.

MWITO WA HARAMBEE

Mwito wa harambee umetuunganisha pamoja katika jitihada za kutosheleza mahitaji yetu ya vituo vya afya, maji, ujenzi wa barabara za mashambani, nyumba za mikutano, mabwawa ya kuogeshea ng'ombe, shule za msingi, shule za ufundi za vijijini, shule za ufundi za sekondari, vyuo vya masomo ya kazi, na kadhalika.

Serikali ya KANU itaendelea kuhimiza mwito wa harambee. Upangaji na utekelezaji wa maendeleo yalioanzishwa kwa njia ya harambee yataunganishwa na ya Serikali ili yapate kutekelezwa kwa njia bora na kamati za maendeleo za wilaya.

Serikali na Chama cha KANU itawahimiza waanzilishi wa mipango ya harambee wahakikishe kwamba kuna pesa za kutosha kuendesha na kusimamia mipango hiyo.

MASHIRIKA YA SERIKALI

Kuna mashirika ya Serikali 147 yaliyoanzishwa kufuatia kanuni za Bunge ili kutimiza mahitaji maalum.

Pia kuna kampuni 47 za Serikali ama mashirika yake, Serikali ina kampuni 36 ambazo ina zaidi ya nusu ya hisa, na kampuni 93 ambazo Serikali ama mashirika yake yana hisa chache. Nia ya Serikali ni kuwapatia wananchi kazi zinazofanywa na wageni na kuongoza uchumi wa nchi yetu kwa njia inayofaa. Katika kutimiza nia hiyo, Serikali ililazimika kuanzisha mashirika ya biashara kwa kununua hisa.

Serikali inanua kuchunguza kwa makini shughuli za mashirika yake ili kuona ikiwa:

- (i) Mashirika na kampuni za Serikali ni muhimu kwa maendeleo na kurekebisha mwenendo wa kampuni za watu binafsi.
- (ii) Nia na kusudi za mashirika na kampuni za Serikali zimetimiza ili kampuni na mashirika hayo yavunjwe.
- (iii) Wajibu wa mashirika na kampuni unaoweza kutimizwa na wizara.
- (iv) Wajibu wa mashirika na kampuni za Serikali unaoweza kutimizwa kwa njia bora zaidi na kampuni za watu binafsi, bila kuihatarisha rasilmali ya Serikali mikononi mwa wageni.

Serikali ya KANU imeshatoa maongozi yatakayofuatwa na mashirika ya Serikali katika kuchagua, kutayarisha na kuteua mipango ya maendeleo iliyo muhimu.

Mipango ya uchumi ya mashirika ya Serikali na makisio ya matumizi ya pesa yataunganishwa na mipango ya Serikali ili kuhakikisha kwamba misaada yote ya pesa inatumiwa kufuatia maongozi ya Serikali ya kugawa ipasavyo mapato yetu kwa Serikali, vyama vya ushirika na kampuni za watu binafsi.

SERIKALI ZA WILAYA

Mabaraza ya wilaya, manispaa na miji yana wajibu muhimu katika kuhifadhi, kuimarisha na kupanua demokrasia.

Nia na wajibu wetu ni kuimarisha mabaraza hayo yaweze kukamilisha mipango yao ya maendeleo kulingana na maongozi ya Serikali.

Mabaraza ya wilaya yanaweza kutimiza wajibu huo kwa njia inayofaa yakiwa na uwezo wa kupanga matumizi ya pesa za mipango yao ya maendeleo.

Hatua zifuatazo zitafuatwa kutimiza wajibu wa mabaraza hayo :

- (i) Kamati za maendeleo ya wilaya zitasimamia barabara za sehemu za mashambani. Wakuu wa wilaya wataunganisha mipango ya kamati hiyo.
- (ii) Watumishi wa mabaraza ya wilaya wenye vyeo vya juu wataongozwa na masharti ya halmashauri ya kuajiri watumishi wa Serikali. Idadi na aina ya wafanyikazi wa mabaraza ya wilaya itachunguzwa na kupitishwa na Serikali.
- (iii) Serikali itatoa maongozi kuhusu mapato na kiwango cha ushuru kinachoweza kutozwa na mabaraza ya wilaya. Kila mwaka Serikali itapitisha mipango ya mapato ya mabaraza hayo na kiwango cha ushuru. Utaratibu huo utahakikisha kwamba juhudi za kuongeza mapato ya baraza za wilaya hazitazotesha mipango ya kilimo, viwanda ama biashara wala kuhitilafiana na maongozi ya Serikali.
- (iv) Mapendekezo haya yatasababisha kupunguzwa kwa kiasi cha misaada inayotolewa na Serikali kusaidia baraza za wilaya. Misaada ya Serikali itahitajiwa kupewa tu wilaya ambazo hazina mapato ya kutosha na ambazo hazina uwezo wa kutosheleza mahitaji ya wananchi.

MAENDELEO YA SEHEMU ZA MASHAMBANI

Sehemu kubwa ya wananchi ambayo ni jumla ya asilimia themanini ya wana Kenya wote, wanaishi sehemu za mashambani. Asilimia sitini ni wakulima na wafugaji, na asilimia ishirini wana mapato mengineyo.

Maendeleo ya sehemu za mashambani yamekuwa msingi wa mipango yetu yote ya maendeleo tangu wakati tulipojinyakulia uhuru. Serikali itazidisha ushirikiano wake na wananchi katika kuchagua, kupanga, kutekeleza na kusimamia mipango ya maendeleo.

Wilaya zitasimamia maendeleo yote ya sehemu zao. Kamati ya viongozi wa idara za Serikali wilayani itaanzishwa. Kamati hiyo itaongozwa na mkuu wa wilaya na itapewa wajibu wa kusimamia, kuongoza na kutekeleza mipango yote ya maendeleo wilayani. Kazi ya kamati hiyo itakuwa ikiongozwa na kamati ya maendeleo ya wilaya.

Kuhakikisha kwamba kamati ya maendeleo ya wilaya itatimiza wajibu wa kupanga, kuongoza na kutekeleza mipango ya maendeleo, hatua zifuatazo zitafuatwa:

- (i) Wengi wa wafanyikazi walio na ujuzi maalum wanafanya kazi za usimamizi mikoani na wizarani. Wafanyikazi hao watapelekwa wilayani kufanya kazi zinazolingana na ujuzi wao. Wafanyikazi wengine wataendelea na kazi zao mikoani na kutoa usaidizi wilayani hadi wakati zitakapopata wafanyikazi walio na ujuzi unaotakikana. Mipango hiyo itasababisha kupunguzwa kwa idadi ya wafanyikazi wa makao makuu ya mikoa.
- (ii) Mkuu wa wilaya, aliye msimamizi wa maendeleo anatakiwa kuwa mtu asiyehusika na siasa, kiongozi aliyehitimu na mwenye ujuzi.
- (iii) Kamati ya viongozi wa idara za Serikali wilayani itapanga matumizi ya pesa za wilaya. Mpango huo utalazimu kuimarishwa hazina za wilaya ambazo zitaongezewa uwezo wa kuhifadhi hesabu za matumizi ya pesa.

- (iv) Kamati ya maendeleo ya wilaya ndiyo pekee itakayokuwa na uwezo wa kupekua na kupitisha ama kubadilisha mipango na makisio ya matumizi ya pesa. Kamati hiyo itachunguza maendeleo, mipango ya uchumi na makadirio ya matumizi ya pesa ambayo yametayarishwa na kamati ya viongozi wa idara za Serikali. Wenyekiti wa baraza za wilaya, kamati za maendeleo ya tarafa na wawakilishi wa mitaa watakuwa wanachama.
- (v) Kamati za maendeleo ya tarafa zitaimarishwa na kuongezwa uwezo wa kusimamia kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo. Wenyekiti wa kamati hizo watatakiwa wahu-dhurie mikutano ya kamati ya viongozi wa idara za Serikali wakati inapojadilia mipango yao ya maendeleo.
- (vi) Makisio ya matumizi ya pesa yatatarishwa na kila wilaya na kupelekewa wizara zinazohusika baada ya kupitishwa na mkuu wa wilaya. Makisio ya matumizi ya pesa za wizara yatapangiwa kila wilaya.
- (vii) Idhini ya matumizi ya pesa kwa mipango ya uchumi inayotolewa na mikoa sasa itatolewa na wilaya. Hazina za wilaya zitakuwa na wajibu muhimu wa kutoa idhini hiyo katika sehemu zilizo na benki za biashara.
- (viii) Mambo muhimu katika utekelezaji wa maendeleo ya sehemu za mashambani yanayohitaji ushirikiano, kama kutumia magari na kuyatengeneza yanapoharibika, yatafanywa chini ya usimamizi wa mkuu wa wilaya.

KILIMO NA MAJI

Taifa letu sasa linajitegemea kwa mazao ya kilimo, nyama na maziwa.

Nia yetu sasa ni lazima iwe ya kuendelea kujitegemea, pia itakuwa muhimu kupata mazao zaidi ya kuuzia nchi za nje.

Mpango wa kujenga ghala za nafaka kote nchini utaendelea mpaka ukamilishwe.

Serikali ya KANU itaendelea kustawisha jitihada za kuuza mazao ya kilimo.

Nchi yetu imebarikiwa kuwa na ardhi yenye rutuba. Kwa sababu tuko karibu na Mashariki ya Kati na Ulaya tuna nafasi nzuri ya kuziuzia nchi hizo bidhaa zetu.

Matokeo ya vituo vya utafiti wa nyasi, mbegu na mifugo bora lazima yaenezwe kwa wakulima ili wapate kuongeza mazao yao.

Serikali itaendelea kuwapatia wakulima wadogo bei nzuri, masoko, mbegu bora, mbolea na vifaa vinginevyo, huduma za Serikali katika sehemu za mashambani na kuhakikisha kwamba wanalipwa papo hapo kwa mazao yao.

Serikali itaendelea kuwatia moyo wakulima na kuhakikisha kwamba wanalipa mikopo yao.

Serikali ya KANU itaendelea kuzingatia maongozi ya kupatia kila mwananchi maji safi.

Kulingana na juhudi hizo, jambo muhimu ni kwa wananchi kuendelea na juhudi zao za harambee na pia kulipia sehemu ya gharama za maji hayo.

Serikali ya KANU itaendelea na mipango ya kujenga visima, maboma ya maji, mitaro na mifereji ya maji kwa manufaa ya binadamu na mifugo katika sehemu zilizo kavu.

Mashirika yanayostawisha sehemu ya Ziwa Victoria, bonde la Kerio, mito ya Tana na Athi yatazidisha mipango yao ya kutumia maji ya sehemu hizo kwa kunyunyiza mashamba, matumizi ya nyumbani na stima.

VYAMA VYA USHIRIKA

Zaidi ya nusu ya wananchi wa Kenya wanahusika kwa njia mbalimbali na vyama vya ushirika.

Kuna vyama 2,652 vya ushirika vilivyo na zaidi ya washiriki milioni moja na mia saba elfu.

Hii inaonyesha kwamba asilimia hamsini na mbili ya jamii milioni tatu na mia moja elfu wanahusika na vyama vya ushirika.

Katika sehemu za mijini, zaidi ya nusu ya wafanyikazi wanaopokea mishahara ni wanachama wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo.

Katika bidhaa muhimu za kilimo zinazouzwa humu nchini asilimia hamsini na tano zinapitia vyama vya ushirika.

Serikali ya KANU itaendelea kuongezea nguvu juhudi za vyama vya ushirika vinavyouza mazao ya kilimo na kupatia wakulima mikopo ya kununua vifaa.

Vyama vya akiba na mikopo vitasaidiwa katika juhudi za kutumia akiba zao kwa mipango ya uchumi. Ingawa Serikali itatoa maongozi, vyama hivyo vitakuwa huru kuchagua mipango yao.

Serikali ya KANU itaimarisha ujuzi wa makarani wa kutunza pesa, wakaguzi wa pesa, watunza vifaa, wasimamizi na wafanyikazi wengine.

Serikali ya KANU itaendelea kusisitiza kwamba faida ya usimamizi mwema wa ushirika ni kuongezeka kwa malipo yanayofaidi wanachama.

Ni lazima washiriki iwalipe haki zao ipasavyo, na hesabu za matumizi ya pesa zikaguliwe kama inavyotakikana na wanakamati wachaguliwe kufuatia masharti ya vyama vya ushirika.

BIASHARA NA VIWANDA

Dhamira yetu ya kustawisha biashara, viwanda na kilimo kwa watu binafsi itatiliwa mkazo.

Tunaamini kwamba mtu anayeona faida kwa kazi atakayofanya atajitolea kwa moyo wake wote.

Serikali ya KANU itaendelea na jitihada zake za kuwapatia wananchi kazi zinazofanywa na wageni.

Tutaendelea kushirikiana na wenye rasilmali kutoka nchi za nje waendeleo na mipango yao ya uchumi humu nchini.

Kampuni za biashara na viwanda zinazoozongeza nafasi nyingi za kazi na ambazo zinatumiya vifaa zaidi kutoka humu nchini zitasaidiwa kwanza.

Tutazidisha ushirikiano wetu na walio na rasilmali kutoka nchi za nje ambao wana moyo wa kuungana mkono na wananchi au kuwapatia hisa za kampuni zao.

Serikali ya KANU itashirikiana na wenye biashara na viwanda kupanua na kuzidisha mipango ya kuelimisha wananchi ili waweze kufanya kazi za kusimamia kampuni hizo.

Shughuli za utalii zinatuletea kiasi kikubwa cha pesa za nchi za nje. Tutaimarisha shughuli hizo na kuhakikisha kwamba Taifa letu linanufaika.

MAWASILIANO

Tumekaribia kukamilisha kujenga barabara za lami zinazounganisha Kenya na nchi jirani, barabara za kuunganisha makao makuu ya wilaya na mikoa, na barabara za kuunganisha wilaya zilizo jirani.

Tutatilia mkazo ujenzi wa barabara za sehemu za mashambani ili kuwawezesha wakulima wauze nafaka zao na kupata vifaa muhimu.

Mipango mikubwa iliyoanzishwa na Shirika la Posta na Mawasiliano ya kujenga ofisi za posta na simu itazingatiwa kwa dhati.

Mpango wa ukaguzi wa idadi na hali ya viwanja vya ndege vikubwa na vidogo umekamilishwa. Nia yetu ni kuvistawisha viwanja hivyo.

Tutakamilisha mpango wa kuongeza magari ya moshi, mabehewa na njia za magari ya moshi ya Shirika la Reli.

Tutakipanua kiwanda cha Shirika la Reli cha kutengeneza vifaa ili kiweze kutengeneza aina mbalimbali ya vifaa vinavyohitajika humu nchini.

ELIMU

Serikali ya KANU iko karibu kutimiza ahadi yake yakupatia kila mtoto elimu ya msingi ya bure.

Idadi ya watoto wa shule za msingi imefikia milioni nne na nusu ambayo ni asili mia tisaini na nane ya watoto wote walio-timiza umri wa kuingia shule za msingi.

Lengo letu sasa ni kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata elimu ya bure kwa miaka minane ya kwanza. Taratibu ya masomo itarekebishwa ili watoto wanaotoka shule baada ya miaka minane ya kwanza wawe na uwezo na nia ya kufanya kazi zozote zitakazokuweco.

Kuanzia Januari, 1985 tutaanzisha mpango wa elimu ya miaka minane ya elimu ya msingi, minne ya sekondari, na minne ya chuo kikuu.

Wazazi wanalazimika wajenge madarasa yanayohitajika kwa haraka.

Idadi ya wanafunzi wa shule za sekondari imefikia 500,000. Katika miaka ijayo tutatilia mkazo elimu ya ufundi, na tutaongeza idadi ya shule za ufundi za vijijini na za sekondari.

Taratibu za masomo, mitihani na vyeti vya kuhitimu vitalingani-shwa katika vyuo mbalimbali vya ufundi ili wanafunzi wanaosomea masomo ya aina moja wapatiwe kazi bila ubaguzi.

Shule za Taifa za elimu ya sanaa pamoja na shule za ufundi za harambee zitatumiwa kwa ukamilifu kutoa aina ya ujuzi unaotakikana kwa maendeleo yetu.

Mipango ya ujenzi wa chuo kikuu cha pili inaendelea. Chuo hicho kikuu pamoja na Chuo Kikuu cha Nairobi vitatilia mkazo kufundisha ujuzi unaotakikana zaidi humu nchini.

Wazazi na wanafunzi wanaopokea elimu ya sekondari na ya chuo kikuu watashirikiana na Serikali kulipia sehemu ya gharama za elimu hiyo. Kwa sababu hiyo mipango ya Serikali ya kutoa mikopo ya elimu ya juu inachunguzwa. Mpango wa elimu ya watu wazima utaendelea mpaka ukamilishwe.

AFYA

Serikali ya KANU itazidi kuongeza mipango ya kuelimisha jamii kuhusu vyakula bora vinavyofaa kwa afya, na kuwapatia maji safi, ili kuzuia na kumaliza magonjwa ya kuambukiza kama kipindupindu, polio, ukambi, malaria na kadhalika.

Mipango ya Serikali ya kujenga na kuvipatia vifaa vituo vya afya itaunganishwa na mipango ya harambee.

Ahadi ya kujenga hospitali za kisasa katika kila wilaya itakamilishwa haraka iwezekanavyo.

Mipango wa kuongeza elimu ya madaktari, wauguzi, wakaguzi wa afya na kadhalika utatekelezwa kulingana na uwezo wetu.

Tutaendelea kuhimiza afya ya jamii na kuelimisha wananchi jinsi ya kuepuka maradhi.

VYAMA VYA WAFANYIKAZI

Katiba na sheria za nchi yetu zinawapa wafanyikazi uhuru wa kujiunga na vyama vya wafanyikazi.

Serikali ya KANU itazidi kuimarisha Shirika la Wafanyikazi la Taifa na vyama vya wafanyikazi ili wanachama wao wafanye kazi zao kwa bidii.

Wafanyikazi watatiwa moyo kuanzisha vyama vya akiba na mikopo, na kujiunga na kampuni za biashara na viwanda kwa kununua hisa.

Serikali ya KANU itahitaji Shirika la Wafanyikazi la Taifa litosheleze mahitaji ya wanachama wake, kwa hivyo shirika hili litahakikisha kwamba uchaguzi unafanywa inavyopasa, ukaguzi wa hesabu za pesa unachapishwa, na akiba za wanachama zinatumiwa katika mipango yenye faida.

ULINZI NA USALAMA WA NCHI

Kenya inathamini kuishi kwa amani na nchi zilizo jirani, na Serikali ya KANU itaendelea kustawisha uhusiano mwema na nchi jirani.

Serikali ya KANU itaendelea kuhifadhi amani humu nchini na kutunza mali na maisha ya wananchi.

Tuna wajibu wa kulinda uhuru na utu wetu kwa kuwa tayari kila wakati kuitetea nchi yetu na kuwaangamiza wahalifu na watu wabaya miongoni mwetu.

Kwa hivyo, Serikali ya KANU itahakikisha kwamba majeshi yetu na polisi wako tayari kila wakati na wana vifaa vya kutosha kupambana na maadui wetu. Hata hivyo, kwa sababu nchi yetu bado inaendelea, inatubidi tutumie tu schemu ya mapato inayotosha kwa shughuli hizo. Chama cha KANU kitazingatia maongozi yake ya kutumia mapato yetu kwa njia inayofaa kustawisha maendeleo ya wananchi wa Kenya.

AFRIKA

Serikali ya KANU itaendelea kutimiza ahadi ya kufuata masharti ya Shirika la Umoja wa Nchi Huru za Afrika na vyama vyote vya Kiafrika vinavyotafuta njia za kuinua maisha na kuunganisha Waafrika.

Tunaamini kwamba Waafrika wenyewe wanaweza kusuluhisha matatizo yao kwa njia ya amani.

Tunaunga mkono jitihada za Shirika la Umoja wa Nchi Huru za Afrika za kustawisha ushirikiano wa kiuchumi kufuatia mkataba wa Lagos.

Serikali ya KANU itaendelea kuwaunga mkono ndugu zetu wa Namibia na Afrika Kusini katika jitihada zao za kujikomboa.

Tunaunga mkono mpango wa biashara bila vikwazo kati ya nchi za mashariki na kusini mwa Afrika, na tutafanya kila tuwezavyo kuhakikisha kwamba mpango huo umefaulu.

UHUSIANO NA NCHI ZA KIGENI

Serikali ya KANU itaendelea kuzingatia maongozi yake ya kutofungamana na upande wowote.

Tutaendelea kushirikiana na nchi nyingine zinazostawi katika jitihada za kutafuta ushirikiano mwema wa kiuchumi. Ushirikiano huo utasawazisha mapato, biashara, uongozi na usimamizi wa mashirika ya biashara ulimwenguni.

Serikali ya KANU itaendelea kutafuta uhusiano mwema na mataifa yote.

WIMBO WA TAIFA

1.

Ee Mungu nguvu yetu
Ilete baraka kwetu.
Haki iwe ngao na mlinzi
Natukae na undugu
Amani na uhuru
Raha tupate na ustawi.

2.

Amkeni ndugu zetu
Tufanye sote bidii
Nasi tujitoe kwa nguvu
Nchi yetu ya Kenya,
Tunayoipenda
Tuwe tayari kuilinda.

3.

Natujenge taifa letu
Ee, ndio wajibu wetu
Kenya istahili heshima
Tuungane mikono
Pamoja kazini
Kila siku tuwe na shukrani.

NATIONAL ANTHEM

1.

O God of all creation
Bless this our land and nation
Justice be our shield and defender,
May we dwell in unity,
Peace and liberty;
Plenty be found within our borders

2.

Let one and all arise
With hearts both strong and true.
Service be our earnest endeavour,
and our Homeland of Kenya,
Heritage of splendour,
Firm may we stand to defend.


3.


Let all with one accord
In common bond united,
Build this our nation together
and the glory of Kenya
The fruit of our labour
Fill every heart with thanksgiving.



RAIS AJENGA NCHI!!

FUATA NYAYO!!





HAKI

IWE NGAO

NA MLINZI